## FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL9

## KISWAHILI PAPER 2 QUESTIONS

# 1. UFAHAMU (Alama 15 )

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

1. Katika karne hii, juhudi zetu za kushughulikia changamoto za usalama zimeimarishwa zaidi kwa matumizi ya teknolojia. Kuimarika kwa ufungaji milango, matumizi ya vifaa vya kamsa, njia za kisasa za utambuzi, utafiti na uchunguzi wa kiuhalifu ni baadhi tu ya maendeleo yaliyoafikiwa na jamii ili kujihami. Sasa hivi huduma zinazotolewa na polisi kwa umma zimewafikia watu kwa njia rahisi. Hata hivyo, maendeleo haya ya kiteknolojia yamehusishwa na hatari fulani. Baadhi ya mifumo inaweza kutumiwa vibaya au ikawa na athari zisizotarajiwa kama vile kumdhuru mtu asiyekusudiwa

Matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuukabili uhalifu wa jinai si suala geni. Tangu kuvumbuliwa kwa kikosi cha askari polisi katika karne ya kumi na tisa, utendakazi na maendeleo yake yamepimwa kwa kigezo cha kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika harakati za utoaji huduma kwa raia. Tumeshuhudia maafisa wetu wakitumia vifaa vya utambuzi kwa alama za vidole na matumizi ya vifaa visivyotumia nyaya katika mawasiliano. Lakini kutokana na kuimarika kwa ubunifu wa wahalifu, pana haja ya vikosi vyetu kujipiga msasa zaidi ili kuzuia au kuzima kabisa njama za kihalifu. Matumizi ya teknolojia katika kuzuia visa vya uhalifu yameanza kukubalika na wanajamii kama sehemu ya maisha yao. Leo hii kuna vifaa vya kuchunguza iwapo mtu ana kifaa chochote cha chuma hususan silaha ndogondogo wakati aingiapo kwenye kumbi za umma au anapoabiri magari ya uchukuzi wa umma. Kifaa hiki kimezuia pakubwa uhalifu wa utekaji nyara uliokuwepo awali hasa miongoni mwa magari ya umma mijini. Aidha vifaa vya kudhibiti kasi ya magari vimeimarisha usalama barabarani. Uwekaji wa taa za umeme kwenye viunga vya miji huuhakikishia umma usalama wao na vilevile kuchangia kuwafichua wavamizi.

Kamera za siri kwenye ofisi za kibinafsi, majengo ya umma na kwenye baadhi ya barabara za miji mikuu huwa hifadhi ya matukio anuwai na hivyo kuwa muhimu wakati wa kesi zinazohusisha uvamizi au uhalifu mwingine wowote. Vifaa vidogo vinavyotumia mawimbi ya kielektroniki na ambavyo hutiwa mifukoni ni muhimu wakati wa mawasiliano ya dharura. Huwasaidia sana watu wenye umri mpevu ambao huwa ni windo jepesi la wahalifu. Aidha huwapa hakikisho la kuwa huru kuyaendesha maisha yao kinyume na awali ambapo maisha yao yalitawaliwa na unyanyapaa baada ya kusikia au kuhusika katika visa vya uhalifu. Kwa sasa teknolojia inayotumia miale kufichua silaha haramu zilizofichwa au kumtambua mtu anayenuia kupenyeza mihadarati kwa kumeza vidonge inagonga ndipo. Njia hii hufanya hivi bila kumkaribia mshukiwa na kuepuka hali ya kuhatarisha maisha ya afisa wa ukaguzi. Aidha huwezesha mshukiwa kutambulika mara moja na hatari husika <u>kutadarukiwa</u> bila ajizi.

Licha ya ufaafu wa teknolojia ya kisasa katika kuzuia au kuzima kabisa visa vya uhalifu, athari zake hasi zimeweza kushuhudiwa. Kwa mfano matumizi ya vifaa vya kwenda kwa kasi kuwafuata wahalifu yanaweza kuwa hatari kwa mtumiaji, mshukiwa au hata raia asiyehusika. Kifaa cha kuzima kasi ya magari kwa mbali kinaweza kulisimamisha gari ghafla na kusababisha maafa makubwa. Matumizi ya mwangaza mkali au gesi kama njia ya kumdhiti mhalifu yanaweza kusababisha ulemavu wa kuona au hata kupumua. Baadhi ya vifaa ambavyo u hutumia miale vinaweza kuwa na athari ya kudumu na hata kusababisha maradhi ya kansa. Inapendekezwa kuwa matumizi ya teknolojia kuangamiza uhalifu yazingatie haki za binadamu.Aidha njia husika iwe nafuu, pawe na uwazi na uwajibikaji katika matumizi yake na vilevile matumizi yake yazingatie maadili.

a) Pendekeza kichwa mwafaka cha habari hii. (alama 2)
……………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………
…………………………………………

b) Eleza jinai changamoto za usalama zimeshughulikiwa katika karne hii. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………

c) Onyesha jinsi teknolojia imeimarisha usalama katika sekta ya usafiri. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

d) Eleza manufaa mawili ya kutumia miale kama njia ya kuzuia uhalifu. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

e) Teknolojia ya kisasa katika kuukabili uhalifu yaweza kuletea watu matatizo .Thibitisha (alama 3)

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

f) Katika kuteua mbinu ya kuukabili uhalifu, jamii yafaa kuongozwa na nini? (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………

g) Elezaa maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

i) Kujipiga msasa ……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

ii) Unyanyapaa ……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

iii) Kutadarukiwa ……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

## 2. MUHTASARI (Alama 15 )

### Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

2. Wanawake wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi zinazoendelea ni baadhi ya watu waliotopea na kubobea katika uchochole mkubwa. Jumla ya idadi kubwa ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake wanaoishi kwenye maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu pamoja na kuwako kwa matatizo ya kiuchumi duniani. Kadhalika matatizo mengine ni mitafaruku na vita vya kikabila, majanga ya kiasili mathalan mafuriko ya ukame na milipuko ya volkano. Usisahau pia kuwa kuna uhalifu wa kimazingira, mabadiliko ya desturi na kusambaratika kwa familia na misingi yake. Tatizo Iingine ni kuwa kuna kuongezeka kwa hali ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza familia zinazosimamiwa na wanawake (ambao tumewataja kuwa wanakumbwa na umaskini mkubwa). Wanawake wanaoishi mashambani wanakumbwa na makubwa. Kwanza, kama maskini wanaishi katika mazingira magumu. Vile vile kama wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na kitamaduni yanayowadharau na kuwapuuza wanawake na mchango wao katika maendeleo. Tatu kama viongozi wa familia, hasa wanaolea na kutunza jamaa za mzazi mmoja, wanapambana na uongozi wa familia pamoja na uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi wowote katika majukumu kama haya bali wanalazimika kupambana nayo peke yao. Kutokana na hayo yote wanawake hawapati nafasi nzuri kushiriki katika maamuzi ya maswala yanayowahusu. Maswala mengi

yanaamuliwa na wanaume pasipo kuwahusisha wanawake.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa njia mbalimbali. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii, taifa na familia. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa wanawake ndio chanzo cha nguvukazi kwani ni wao na watoto wao wanaotekeleza kazi nyingi hasa za nyumbani na mashambani. Mara nyingi huwa na uwezo bora wa kutunza chochote walichonacho kuliko wenzao wanaume

Kifamilia wanawake wa mashambani wanashughulika mchana kutwa katika hali ngumu ya hewa aidha jua kali au mvua huku wameeleka wanao migongoni wakilima mashamba ili kupata chakula kwa familia zao. Jukumu la kuandaa chakula nyumbani bado linaachiwa wale wale wanawake wanaokizalisha mashambani.

Jambo lisilopingika ni kwamba wanawake wanatekeleza majukumu makubwa na muhimu katika kizazi cha binadamu na ndio hasa mihimili ya jamii yoyote staarabu. Kwa hivyo, ni kinaya kitupu kudhalilisha wanawake. Mataifa mengi yaliyoendelea ni yale yaliyoondoa vikwazo vyote mbele ya wanawake na kuwaacha watekeleze wajibu wao.Kadhalika wanaume wa huko wanawaona wanawake kuwa wenzao katika kujenga jamii wala sio watumwa au watumishi wao wanaoumia na kutumikishwa kama vifaa na bidhaa. Inafaa jamii zinazodunisha wanawake zitambue kuwa ubaya wa tendo hili sio tu kudumaza maendeleo yake bali pia kutoa mfano mbaya kwa vijana ambao wataendeleza ukandamizaji huu kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, jamii inawajibika kutenda lililo sawa kwa kuwapa hadhi wanawake wote.

a) Bila kubadilisha maana fupisha aya tatu za kwanza. (Maneno 75-80). (Alama 8)

Matayarisho

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

Jibu

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................
.....................................................................

.............................................................................................................................................

……………………………………………………………………

b) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, pambanua hoja muhimu (maneno 70 -75) (alama 7)

Matayarisho

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

Jibu

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40 )

3. a) Taja aina mbili za matamshi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

b) Yakinisha sentensi hii. (alama 2)

Hajanivunjia dirisha wala kuniibia.

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………

.........................................................

c) Tambua vihusishi katika sentensi hii. (alama 2)

Mto Lucha ulikuwa karibu na soko ulijaa hadi pomoni

.........................................................................................................................................................
.........................................................

.........................................................................................................................................................
.........................................................

d) Changanua sentensi ifuatayo kwa mabawi. (alama 4)

Walijenga nyumba nzuri sana jana

.........................................................................................................................................................
.........................................................

.........................................................................................................................................................
.........................................................

e) Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi hii. (alama 2)

Ndovu aliuawa na wawindaji haramu nami nikawaripoti.

.........................................................................................................................................................
.........................................................

.........................................................................................................................................................
.........................................................

f) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha utenzi. (alama 1)

.........................................................................................................................................................
.........................................................

g) Andika kinyume cha sentensi hii. (alama 3)

Je, watu walio matajiri huzaliwa na baraka?

.........................................................................................................................................................
.........................................................

.........................................................................................................................................................
.........................................................

h) Tunga sentensi moja ukionyesha maana tofauti ya vitate vifuatavyo: (alama 2)

Bua / pua

.........................................................................................................................................................
.........................................................

.........................................................................................................................................................
.........................................................

i) Eleza matumizi mawili ya herufi mlazo (italiki) (alama 2)

.........................................................................................................................................................

……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

j)(i) Vitenzi sambamba ni nini? (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

(ii) Tunga sentensi ukitumia vitenzi sambamba (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

k) Bainisha aina za nomino katika sentensi hii. (alama 3)

Kulia kwa Bi. Oduori kulileta huzuni.

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

l) Andika katika hali ya ukubwa. (alama 2)

Mwanamke huyo alizaa watoto watatu.

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

m) Onyesha vishazi huru na vishazi tegemezi. (alama 2)

Serehangi aliyeshikwa alikuwa mkorofi.

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

n) Badili sentensi hii katika hali ya kutendeana. (alama 2)

Si vizuri mtu kumwibia mwenzake simu.

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

p)

(i) Ngeli ni nini? (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

(ii) Taja mianzo miwili tofauti ya majina katika ngeli ya U –ZI. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

p) Ainisha viambishi tamati katika neno hili. (alama 1)

Awaambiaye

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

q) Bainisha matumizi ya 'po' katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mgeni alipofika alionyeshwa walipo

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

r) Onyesha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Wakulima hao wamekuwa wakipanda mashamba yao vyema kila mara.

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

s) Ainisha mofimu hizi. (alama 2)

(i) Mende……………………………………………………………………………………………………………
………………………………

(ii) Mpwa……………………………………………………………………………………………………………
………………………………

## 4. ISIMUJAMII (Alama 10 )

4. a) Fafanua istilahi zifuatazo: (alama 2)

(i) Pijini

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

ii) Krioli

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

b) "…ah.. na kunyamaza nako….ni Caro…….naam, naam. Hujambo?...si…si…neno….naam. Mjomba Fadhili amezidiwa si wa maji…..eh! Kweli?. ... mwuguzi mkuu amedhihirisha……Yes…..ok…yeah….Ala! pesa zikaisha.

i) Tambua sajili ya muktadha huu. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

ii) Eleza sifa sita za sajili hii. (alama 6)

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………